# I.Habari kuhusu bidhaa

# Mada ya 23

# Mapendekezo ya upanzi wa baadhi ya mimea mikuu nchini Nigeria

# JARIDA LA UHAKIKA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## **Mada ya 23:** Mapendekezo ya upanzi wa baadhi ya mimea mikuu nchini Nigeria

Kila mmea una **mapendekezo fulani ya mbegu**. Katika jedwali lifuatalo kuna mapendekezo ya mbegu kwa mimea mikuu nchini Nigeria. Mkulima anapokuja dukani kununua mbegu, waweza kumshauri kiasi cha mbegu anachofaa kununua na vile atakavyozipanda mbegu hizo. Kama atafuata ushauri wako basi mazao yake yatakuwa ya juu.

Katika jedwali utapata habari ifuatayo:


- **Mmea**: Huu ndio mmea ambao mapendekezo itatumiiwa kwake.
- **Kiwango/kipimo cha mbegu**: Hiki ndicho kiasi cha mbegu zinazohitajika kupandwa katika hekta moja ya shamba na wakulima ili wapate mazao ya juu kabisa.
- **Nafasi kati ya mmea mmoja na mwingine**: Hii ndio nafasi kwa centimita iliopendekezwa kutumia kati ya mimea.

| | **Crop** | **Seed rate (kg/ha)** | **Crop spacing (in centimeters)** |
|---|---|---|---|
| 1 | Maize | 20 – 25 | 75 x 25 |
| 2 | Rice | 50 (transplanting)<br>60 (dibbing)<br>80 – 100 (broadcast) | 20 x 20 |
| 3 | Cowpea | 30 – 35 | 75 x 25 |
| 4 | Sorghum | 12 – 15 | 75 x 30 |
| 5 | Millet | 10 – 12 | 75 x 30 |
| 6 | Soybean | 50 | 75 x 10 |
| 7 | Groundnut | 40 | 75 x 20 |
| 8 | Cotton | 20 – 25 | 90 x90 |
| 9 | Cassava | 50 (bundles) | 90 x 90 |
| 10 | Yam | 40,000 (seed yams) | 100 x 100 |
| 11 | Irish Potato | 1,200 | 90 x 90 |
| 12 | Melon | 7 | 200 x 200 |
| 13 | Leafy Vegetables | 0.5 – 0.75 | 10 x 10 |
| 14 | Pepper | 1.0 – 1.5 | 40 x 30 |
| 15 | Tomatoes | 0.6 | 90 x 30 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16 | Onion | 9 | 20 x 20 |

**Kwa mfano:**

Hekta moja ya njugu inahitaji kilo 40 za mbegu, nafasi kati mimea ni centimita 75 katika kulia na kushoto na centimita 20 upande wa mbele na nyuma.



# MWONGOZO

## I. Habari kuhusu bidhaa

## **Mada ya 23:** Mapendekezo ya upanzi wa baadhi ya mimea mikuu nchini Nigeria

**Vifaa vinavyohitajika:**

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Ukanda wa kubandikia

**Muda unaohitajika:** Dakiki 90

**Maandalizi:**

- ☑ Karatasi ya kufungua kurasa ilio na kichwa: *Mapendekezo ya upanzi wa baadhi ya mimea mikuu nchini Nigeria.*
- ☑ Karatasi ya kufungua kurasa ilio na kichwa : *Mapendekezo ya Upanzi* halafu chini yake: *Kipimo/kiwango cha mbegu na nafasi kati ya mimea*.
- ☑ Nakala ya *mapendekezo ya upanzi* ya kila mshiriki

## Mwanzo

**U**sikivu: Waambie washiriki kwamba sasa tumefikia sehemu muhimu sana ya mafunzo yetu.

**K**ichwa: Waambie washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi ya kufungua kurasa ilio na kichwa: *Mapendekezo ya upanzi wa baadhi ya mimea mikuu nchini Nigeria*

**K**usadikika: Elezea uzoefu wako katika uwanja wa mbegu.

**M**alengo: Kueleza vile chati za mapendekezo ya upanzi zinavyotumiwa.

**M**anufaa: Kama waweza kutumia chati ya mapendekezo ya upanzi, unaweza kuwashauri wateja wako kuhusu kiasi cha mbegu


watanunua na vile wanaweza kuzipanda. Kutokana na mapendekezo haya, wakulima watapata mazao ya juu na kurejea kama wateja walioridhika.

**M**welekeo: Katika kipindi hiki, tutaangazia kiasi cha mbegu kinachohitajika kwa kila hekta na nafasi inayofaa kuachwa kati ya mbegu zinapopandwa. Hatutajadili vipengele vingine vya upanzi.

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba kuna vipengele viwili muhimu vya mapendekezo ya upanzi: Kiwango/kipimo cha mbegu na nafasi kati ya mimea.
2. Uliza yeyote kufafanua maana ya kiwango/kipimo cha mbegu. Hiki ni kiasi cha mbegu kinachohitajika kupandwa katika hekta moja ya shamba ili wakulima wapate mazao ya juu sana. Kama kiwango/kipimo cha mbegu ni 30 hii inamaanisha ni kilo 30 zitahitajika kwa hekta moja.
3. Uliza kama yeyote anaelewa nafasi kati ya mbegu mbili. Hii ni nafasi inayopendekezwa kati ya mbegu mbili za mmea. Andika 50 x 30 kwenye karatasi ya kufungua kurasa na uulize maana yake. Hii inamaanisha mbegu zafaa zipandwe na nafasi ya centimita 50 kulia na kushoto na centimita 30 mbele na nyuma.
4. Uliza kama yeyote anaweza kuchora kuonyesha nafasi hiyo.




☆ = Mbegu zilizopandwa

5. Sambaza nakala zilizo na **mapendekezo ya upanzi**. Unda vikundi vya washiriki watatu. Hakikisha kuna mtu anayejua kusoma na kuandika katika kila kikundi. Waeleze kwamba wewe ni mteja na umeingia kwenye duka lao kununua mbegu na unataka ushauri wao. Taja mmea mmoja ulio kwenye chati za mapendekezo na uwapatie muda wa kuangalia kiwango/kipimo cha mbegu na nafasi inayohitajika kati ya mbegu mbili. Uliza kikundi kimoja kukupa ushauri. Ni lazima waeleze vyema ni kilo ngapi za mbegu utahitaji na namna utazipanda.
6. Taja mmea tofauti na muujadili kama mbeleni. Endelea kutaja mimea mpaka makundi yote yashiriki kutoa mapendekezo.

## Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari kwa kuelezea kiwango/kipimo cha mbegu na nafasi kati ya mmea.

**M**aswali**:** Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni

**T**athmini**:** Waulize kueleza kiwango/kipimo cha mbegu na nafasi kati ya mimea.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tumejifunza vile tunaweza kutumia chati za mapendekezo. Wakati ujao mteja akienda kwa duka la bidhaa za kilimo, ushauri bora utapeanwa.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.

# Ushauri wa  kupanda

| | Crop | Seed rate (Kg/Ha) | Crop spacing (in centimeters) |
|---|---|---|---|
| 1 | Maize | 20 – 25 | 75 x 25 |
| 2 | Rice | 50 (transplanting)<br>60 (dibbing)<br>80 – 100 (broadcast) | 20 x 20 |
| 3 | Cowpea | 30 – 35 | 75 x 25 |
| 4 | Sorghum | 12 – 15 | 75 x 30 |
| 5 | Millet | 10 – 12 | 75 x 30 |
| 6 | Soybean | 50 | 75 x 10 |
| 7 | Groundnut | 40 | 75 x 20 |
| 8 | Cotton | 20 – 25 | 90 x90 |
| 9 | Cassava | 50 (bundles) | 90 x 90 |
| 10 | Yam | 40,000 (seed yams) | 100 x 100 |
| 11 | Irish Potato | 1,200 | 90 x 90 |
| 12 | Melon | 7 | 200 x 200 |
| 13 | Leafy Vegetables | 0.5 – 0.75 | 10 x 10 |
| 14 | Pepper | 1.0 – 1.5 | 40 x 30 |
| 15 | Tomatoes | 0.6 | 90 x 30 |
| 16 | Onion | 9 | 20 x 20 |